JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

Multisectoral magazine

AGOSTI 2022 | ISSUE NO 009




## Sensa 2022

## KWA MAENDELEO ENDELEVU

TSHS. 15,000 KSHS. 735 USHS 23,000
www.tz&beyond.co.tz

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania

# BODI
## YA WAHARIRI

**AFISA MTENDAJI MKUU**
Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

**MHARIRI MTENDAJI**
Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA**
Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**
Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

**MWENYEKITI/MLEZI**
Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com

**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com

TZ&BEYOND



# Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU






38 Sensa kuisaidia serikali ya Rais Samia


36 Aina za majengo yatakayohesabiwa


40 Umuhimu wa sensa 2022


33 Sensa ya majengo 2022




46
Mufti tushiriki zoezi la sensa





48
Sheikh Ponda Sensa ni muhimu kwa taifa







65
Anne Makinda aipa thamani sensa





42
Tofauti ya sensa ya 2022 na zilizopita

KCB BANK


Agency Banking
Internet Banking
I-Bank
ATM
Mobile Banking
Mobi
TISS
EFT
TT
E.A Payments
Government Electronics Payments (GEPG)
Let's talk
Internet Banking App
My experience with KCB Bank is that of modern times...

# RAIS SAMIA:

## SENSA *ni* YA KILA MTANZANIA




**sensa ni ya kila mtu ili ifanikiwe, uelimishaji na uhamasishaji ni masuala yanayotakiwa kupewa kipaumbele kuwasaidia wananchi kutoa taarifa**

# Sensa

# 2022

KWA MAENDELEO ENDELEVU



SENSA ya watu na makazi inayotarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu ni ya kihistoria, hii itakuwa ni sensa ya sita tangu kuzaliwa kwa Tanzania mwaka 1964 baada ya kuungana kwa Tanganyika na Zanzibar.

Kimsingi Sensa hii imebeba umuhimu wa kipekee kutokana na kuwapo kwa mabadiliko makubwa ya kiteknolojia, ambayo yatasaidia kufanikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za watuna makazi.

Muandaaji mkuu wa sensa hii ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na dhamana ya kulisimamia jambo hili imeachwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS).

Maandalizi ya suala hili la kitaifa linalofanyika kila baada ya miaka 10 ambapo Sensa ya mwisho kufanyika nchini ilikuwa mwaka 2012, yamekamilika kwa kiwango kikubwa.

Sensa ya mwaka huu itakuwa ni ya Sita kufanyika nchini ikitanguliwa na zile za mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda ndie amepewa jukumu la kuwa kamishna wa Sensa ya Watu na Makazi, akisaidiwa na viongozi mbalimbali wa Bara na visiwani akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

## MAANA YA SENSA YA WATU NA MAKAZI

Zipo tafsiri kadha wa kadha juu ya maana ya Sensa ya Watu na Makazi, miongoni mwake inaelezwa kuwa ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Lakini pia unaweza kuielezea Sensa ya Watu na makazi kama zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

Takwimu zipatikanazo kwenye Sensa ya Watu na Makazi huwa za msingi na ndizo zinazoweza kuanisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum.

Kujua idadi ya watu wa makundi mbalimbali kama vile wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira waliyopo.

Mathalani Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ilihesabu watu 44,928,923 kwa Tanzania nzima, Bara na Visiwani, huku wanawake wakiwa 23,058,933 na wanaume wakiwa 21,869,990.

Sensa hiyo ilionesha dhahiri kuwa wanawake ni wengi zaidi ya wanaume kwa tofauti ya watu 1,188,943. Hii ina maanisha nini?

Wataalamu wa masuala ya vizazi na vifo wanaweka wazi kuwa katika kipindi cha miaka 10 kutoka 2002-2012 kasi ya watanzania kuzaa watoto wa kike imeongezeka, lakini pia kumekuwa na kiwango cha juu cha vifo vya watoto wachanga wakiume.

**Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi la kitaifa linalofanyika kila baada ya miaka 10 ambapo Sensa ya mwisho kufanyika nchini ni ile ya mwaka 2012.**





RAIS SAMIA AKIKABIDHI NEMBO NA VYETI MAALUM KWA WAZIRI MKUU MHE. KASSIM MAJALIWA AMBAE PIA NI MWENYEKITI WA KAMATI KUU YA SENSA

# MADODOSO YA SENSA

- Dodoso refu litakalotumika kuhoji asilimia 30 ya maeneo yote ya kuhesabia watu na Dodoso fupi litakalotumika kuhoji kwenye asilimia 70 ya maeneo yote ya kuhesabia watu.
- Dodoso la Taasisi ambalo ni mahsusi kwa ajili ya wasafiri, waliolala mahotelini/nyumba za wageni, na waliolazwa hospitalini; na
- Dodoso la Wasio na Makazi maalum ambalo ni mahsusi kwa watu wote wanaolala maeneo yasiyo rasmi, kwenye baraza za majengo mbalimbali, kwenye madaraja na maeneo mengine.




RAIS SAMIA SULUHU HASSAN, (KULIA) AKIWA NA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI DKT. HUSSEIN ALI MWINYI KWENYE KUKATA UTEPE KUASHIRIA UZINDUZI RASMI WA NEMBO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI

Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilichozingatiwa kwa wanaume kilikuwa vifo 51 kwa kila watoto wa kiume 1000 ikilinganishwa na vifo 42 kwa kila watoto wa kike 1000 wanaozaliwa hai.

Hata hivyo wadadidisi wa mambo wanaamini upo uwezekano wa sensa ya mwaka huu kuibuka na takwimu za kuridhisha juu ya uwiano huo wa wanawake na wanaume Tanzania.

## UMUHIMU WA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

Hakuna ubishi, sensa ya watu na makazi ni muhimu na umuhimu wa kipekee wa zoezi la mwaka huu ni pamoja na:-

- Kuisadia Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa;

- Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;

- Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;

**Sensa ya mwaka 2022 itakuwa ni sensa ya Sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022

Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

**MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA JARIDA LA TZ&BEYOND TUKO TAYARI KUHESABIWA. SENSA YA WATU NA MAKAZI NI MUHIMU KWA MAENDELEO YA NCHI**

**ASIYEHESABIWA NI WAZI ATAKUWA AMEJINYIMA HAKI YAKE YA KULETEWA MAENDELEO NA SERIKALI, HATUA HIYO ITAMFANYA KUTUMIA HAKI ZA WENGINE.**

**ILI KUEPUKA KUJINYIMA HAKI EWE MTANZANIA JIANDAE KUHESABIWA AGOSTI 23,2022.**

**HATUA HIYO ITAIPA NAFASI SERIKALI YA AWAMU YA SITA INAYOONGOZWA NA KIONGOZI  MAKINI SAMIA SULUHU HASSAN IKULETEE MAENDELEO.**

**USIKUBALI KUPOTOSHWA, TOA TAARIFA SAHIHI, TOA USHIRIKIANO KWA MAOFISA WA SENSA WATAKAOKUFIKIA.**

SENSABIKA KWA MAENDELEO YA TAIFA

# Jiandae kuhesabiwa sensa ya makazi na watu



DONDOO

## SHERIA

Kabla ya Uhuru, Takwimu zilikuwa zinakusanywa kwa kutumia sheria ya Takwimu ya mwaka 1949 (Statistics Ordinance of 1949 – chapter 443). Sheria hii ilikuwa inatumika katika nchi za kikoloni za Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Uganda na Tanganyika. Kupitia sheria hii, Idara ya Takwimu ya Afrika Mashariki ilipewa mamlaka ya kuratibu mfumo (Muundo) wa takwimu za uchumi na jamii wa nchi tatu. Baada ya uhuru mwaka 1961, Mamlaka ya kukusanya, kuhifadhi na kuchapisha takwimu yalitokana na sheria ya Takwimu Na. 33 ya mwaka 1961.





**RAIS SAMIA AZINDUA MKAKATI WA UELIMISHAJI NA UHAMASISHAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022**

# Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

## Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

- . Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano Pato la mtu mmoja mmoja, Pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;
- Taarifa itakayowezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira
- Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia. Takwimu sahihi za Sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

## MADODOSO YA SENSA

**Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo sensa zilizopita itatumia aina mbili kuu za madodoso. Dodoso refu litakalotumika kuhoji asilimia 30 ya maeneo yote ya kuhesabia watu na Dodoso fupi litakalotumika kuhoji kwenye asilimia 70 ya maeneo yote ya kuhesabia watu.**

## MADODOSO MENGINE NI:

- Dodoso la Taasisi ambalo ni mahsusi kwa ajili ya wasafiri, waliolala mahotelini/nyumba za wageni, na waliolazwa hospitalini; na
- Dodoso la Wasio na Makazi maalum ambalo ni mahsusi kwa watu wote wanaolala maeneo yasiyo rasmi, kwenye baraza za majengo mbalimbali, kwenye madaraja na maeneo mengine.



RAIS SAMIA, (KATIKATI) AKIKABIDHI NEMBO YA VYETI MAALUM KWA KATIBU MKUU OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) DKT. JOHN JINGU, KUASHIRIA KUMPA JUKUMU LA KUANZA KAZI HIYO WAKATI WA UZINDUZI RASMI WA NEMBO YA SENSA YA WATU NA MAKAZI AMBAPO SENSA HIYO ITAFANYIKA TAREHE 23 AGOSTI 2022



WAZIRI MKUU, KASSIM MAJALIWA AKIMKABIDHI NAKALA YA KITABU MWAKILISHI WA SHIRIKA LA UMOJA WA MATAIFA LA IDADI YA WATU UNFPA, JACQUELINE MAHON KATIKA UZINDUZI WA KITABU CHA MKAKATI WA USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI




KAMISAA WA SENSA , SPIKA MSTAAFU ANNE MAKINDA AKIZUNGUMZA WAKATI WA UZINDUZI WA MAFUNZO YA WAKUFUNZI WA TEHAMA NGAZI YA TAIFA NA MIKOA KWA AJILI YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022 KATIKA CHUO CHA TAKWIMU AFRIKA MASHARIKI

## UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

**Utekelezaji wa sensa ya watu na makazi hufanyika katika awamu kuu tatu ambazo ni Kipindi Kabla ya Kuhesabu Watu, Wakati wa Kuhesabu Watu na Kipindi Baada ya Kuhesabu Watu.**

- Kipindi kabla ya kuhesabu watu

Kipindi kabla ya kuhesabu watu kinajumuisha uandaaji wa kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa na nyaraka nyingine, utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu na uzalishaji wa ramani, uandaaji wa nyenzo (Madodoso na Miongozo mbalimbali); Uhamasishaji, Sensa ya Majaribio, Kuunda kamati za sensa; kufanya mikutano na wadau wa takwimu; kufanya manunuzi, kufanya uchaguzi wa aina ya teknolojia itakayotumika, kuajiri wadadisi na wasimamizi, usambazaji wa vifaa; na kufanya maandalizi ya Tathmini ya Sensa.



WAZIRI MKUU, KASSIM MAJALIWA AKITETA NA MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR, HEMED SULEIMAN ABDULLA KATIKA UZINDUZI WA KITABU CHA MKAKATI WA USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

### Kipindi cha kuhesabu watu

Kipindi cha kuhesabu watu kinajumuisha kazi kuu na ya muhimu katika zoezi hili la kuhesabu watu.

### Kipindi baada ya kuhesabu watu

Kipindi baada ya kuhesabu watu kinajumuisha uchakataji wa taarifa za Sensa, uchambuzi, utoaji wa matokeo ya awali, usambazaji wa matokeo ya mwisho, uhamasishaji wa matumizi ya takwimu kwa watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

### Maandalizi ya jumla

Maandalizi ya sensa ya watu na makazi 2022 yalianza mwaka 2018, ikiwa ni kutenga maeneo ya kuhesabia watu, kutayarisha **nyaraka muhimu za sensa kama vile madodoso, miongozo, fomu za kudhibiti ubora na kufanya sensa ya majaribio.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA)

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## KUHUSU TMDA

*Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambayo ilikuwa ikijulikana kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, bidhaa za tumbaku, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi.*

*Iliyokuwa TFDA ilibadilishwa jina na kuwa TMDA mnamo tarehe 1 Julai, 2019 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 kupitia Sheria ya Fedha, Na. 8 ya mwaka 2019 ambayo mbali na kubadili jina la Sheria hiyo kuwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219, pia ilihamisha majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi kwenda katika Sheria ya Viwango, Sura 130.*

**DIRA** | Kuwa Mamlaka inayoongoza katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya kwa wote

**DHIMA** | Kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya.

## MAJUKUMU

1. Kusajili na kutoa vibali vya majengo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
2. Kukagua maeneo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
3. Kukagua shehena za bidhaa za dawa, chanjo tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vy forodha na kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa hizi
4. Kutoa vibali vya kuingizia na kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
5. Kusajili bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusiwa kuuzwa katika soko la Tanzania
6. Kudhibiti majaribio ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku na vifaa tiba na kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizi
7. Kudhibiti matangazo ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
8. Kutoa elimu kwa umma

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam au**
**S.L.P 1253 Dodoma**
**Simu: +255 222 450512/450751/452108**
**Simu ya Bure: 0800110084**
**Nukushi: +255 222 450793**
**Barua Pepe: info@tmda.go.tz Tovuti: www.tmda.go.tz**

0800110084 | @tmda_tanzania | @tmda tanzania | www.tmda.go.tz

"TMDA Hulinda Afya ya Jamii"

### Maandalizi muhimu

- Kuandaa Kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022;

- Kutenga Maeneo katika wilaya 5 za mkoa wa Dodoma ambazo ni Bahi, Chamwino, Kondoa, na Chemba; na Wilaya moja ya Mkoa wa Singida (Singida Mjini);

- Kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu inaendelea katika mkoa wa Singida katika wilaya za Manyoni, Ikungi; na mkoani Dodoma katika wilaya za Mpwapwa na Kongwa.

- Kufanyika kwa ziara moja ya kimafunzo nchini Kenya kwa ufadhili wa UNFPA ambao wamefanya sensa ya kidigitali hivi karibuni na kujifunza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kufanya sensa kwa mafanikio. Matumizi ya teknolojia hii itasaidia kupunguza gharama za kufanya sensa na kupunguza muda wa kutoa matokeo ya sensa.

- Kuandaa rasimu ya Dodoso la Sensa na nyaraka nyingine muhimu kama vile miongozo ya kufundishia, miongozo ya makarani wa sensa, miongozo ya wasimamizi wa sensa na miongozo ya waratibu wa sensa mkoa na wilaya.

**Utekelezaji wa sensa ya watu na makazi hufanyika katika awamu kuu tatu ambazo ni Kipindi Kabla ya Kuhesabu Watu, Wakati wa Kuhesabu Watu na Kipindi Baada ya Kuhesabu Watu.**



RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE.DK.HUSSEIN ALI MWINYI AKIFUTILIA HUTUBA YA UZINDUZI WA NEMBO NA TAREHE YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

VIONGOZI WA JUKWAA KUU WAKIFUATILIA HAFLA YA UZINDUZI WA NEMBO NA TAREHE YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022, ILIOZINDULIWA NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE.SAMIA SULUHU HASSAN.(HAYUPO PICHANI)




VIONGOZI WA VYOMBO VYA ULINZI NA USALAMA WAKIMSIKILIZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE.SAMIA SULUHU HASSAN



## MASWALI YATAKAYOULIZWA

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ina moduli kumi na nne ambazo zitatumika kukusanya taarifa za watu na makazi yao nchi nzima.

## MASWALI YATAKAYOULIZWA YATAHUSU

- Taarifa za kidemografia (umri, jinsi, uhusiano, hali ya ndoa, uraia, n.k.);
- Maswali yanayohusu ulemavu;
- Taarifa za Elimu;
- Maswali ya uhamaji, pamoja na taarifa za Watanzania wanaoishi nje ya nchi
- Maswali kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (vitambulisho vya NIDA, Mzanzibari mkazi, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva)
- Shughuli za kiuchumi
- Umiliki wa ardhi na taarifa za TEHAMA
- Taarifa za Uzazi na Vifo vilivyotokea ndani ya kaya
- Vifo vitokanavyo na uzazi
- Hali ya nyumba za kuishi na umiliki wa rasilimali mbalimbali
- Maswali ya kilimo na mifugo
- Mifuko ya hifadhi ya jamii.

**wadadidisi wa mambo wanaamini upo uwezekano wa sensa ya mwaka huu kuibuka na takwimu za kuridhisha juu ya uwiano huo wa wanawake na wanaume Tanzania**

## SENSA YA WATU NA MAKAZI

# 2022

## Takwimu zipatikanazo kwenye Sensa ya Watu na Makazi huwa za msingi na ndizo zinazoweza kuanisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum

BAADHI YA VIONGOZI WAKIMSIKILIZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE.SAMIA SULUHU HASSAN.(HAYUPO PICHANI) AKIHUTUBIA KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA NEMBO YA TAREHE YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022





RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE.DK.HUSSEIN ALI MWINYI AKIKABIDHIWA MAKABRASHA YA SENSA NA KAMISAA WA SENSA YA WATU NA MAKAZI TANZANIA MHE.ANNE MAKINDA



WAZIRI MKUU, KASSIM MAJALIWA AKIAGANA NA MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR, HEMED SULEIMAN ABDULLA BAADA YA KUZINDUA KITABU CHA MKAKATI WA USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022

## Wakati wa zoezi la sensa la mwaka 2012 Tanzania ilikuwa na mikoa 30, kati ya hiyo Zanzibar ilibeba mikoa mitano na Bara ilibeba mikoa 25



VIONGOZI WA SERIKALI NA WANANCHI WAKIMSIKILIZA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE.SAMIA SULUHU HASSAN.(HAYUPO PICHANI) AKIHITUBIA NA KUZINDUA NEMBO NA TAREHE YA SENSA YA WATU NA MAKAZI YA MWAKA 2022,

## TOFAUTI YA SENSA YA MWAKA 2022 NA ZILIZOPITA:

**Katika sensa ya mwaka 2022 inatarajiwa kuwa na vitu vipya kama vile;**

- Kutenga maeneo ya kijiografia ya kuhesabia watu katika ngazi za kitongoji/ mtaa na upatikanaji wa taarifa za kitakwimu katika ngazi za kitongoji/mtaa pamoja na kuwa na mipaka ya kudumu katika ngazi hizo;
- Matumizi ya Vishikwambi (tablets) katika hatua zote za utekelezaji wa sensa kwa lengo la kupunguza gharama;
- Nyongeza ya maswali yatakayowezesha upatikanaji wa taarifa zaidi za kitakwimu ikilinganishwa na Sensa ya Mwaka 2012:-
- Taarifa za kidemografia (umri wakati wa ndoa ya kwanza);
- Maswali yanayohusu ulemavu (Kichwa kikubwa, Mgongo wazi, Kifafa/ Epilepsy, Mbalanga/storiasis na Usonji/autism);
- Maswali ya uhamaji kulingana na mapendekezo ya IOM (International Organization of Migration);
- Maswali kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (vitambulisho NIDA, vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo wadogo, Mzanzibari mkazi, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva);
- Maboresho ya maswali ya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na idadi ya kaya ziliko kwenye sekta isiyo rasmi;
- Umiliki wa ardhi na taarifa za TEHAMA
- Takwimu za nyumba (orodha, hali ya umiliki na aina ya nyumba)
- Maswali ya kilimo na mifugo

## HITIMISHO

**Matarajio ni kujipanga vizuri kwa kutumia rasilimali chache zilizopo ili kukamilisha kwa wakati shughuli zote za maandalizi ikiwamo:-**

- Kazi ya utengaji wa Maeneo ya Kuhesabia Watu katika ngazi ya kitongoji na mtaa ambayo ndiyo msingi wa kufanikisha sensa kwa ubora
- Uandaaji wa nyaraka za sensa;
- Uundaji wa vikosi kazi/units kwa lengo la kugawana majukumu; na
- Ufanyaji wa Sensa ya majaribio tarehe 29 Agosti 2021.


TIB DEVELOPMENT BANK
Your Partner for Growth
Chagua Benki ya Maendeleo TIB
Mshirika Wako Katika Maendeleo
Benki inatoa mikopo kwenye:
• Uendelezaji wa miundombinu
• Maendeleo ya Viwanda
• Uchimbaji wa madini
• Mafuta na Gesi
• Huduma
md@tib.co.tz
www.tib.co.tz

# Nukuu za viongozi



BILA KUWA NA TAKWIMU HUWEZI KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA AJIRA, KUSHUGHULIKIA MATATIZO YA WATU WENYE MAHITAJI MAALUM, KUTOA HUDUMA ZA KIJAMII WALA KUFANYA MAENDELEAO

**RAIS SAMIA SULUHU HASSAN**



WITO WANGU KWENU NYOTE WATANZANIA UKIFIKA WAKATI WA SENSA SOTE TUJITOKEZE KUHESABIWA

**MAKAMU WA RAIS
DKT. PHILIP MPANGO**



MATOKEO YA SENSA YATAIWEZESHA SERIKALI KUPATA TAKWIMU ZINAZOTUMIKA KUAKISI HALI HALISI ILIYOPO NA KUPANGA MIPANGO YA MAENDELEO

**WAZIRI MKUU
KASSIM MAJALIWA**

TUNAAMINI MATOKEO YA SENSA HII YATALISAIDIA BUNGE KUWEZA KUFANYA SHUGHULI ZAKE ZA KUISIMAMIA NA KUISHAURI SERIKALI KIKAMILIFU

**SPIKA WA BUNGE**
**DKT. TULIA ACKSON**



SOTE TUONYESHE UZALENDO WETU KUFANIKISHA ZOEZI HILI MUHIMU KWA TAIFA

**WAZIRI WA FEDHA**
**NA MIPANGO**
**DKT. MWIGULU NCHEMBA**



TUNAPASWA KUJIPANGA VYEMA ILI ZOEZI LA SENSA LIWE LA MAFANIKIO KAMA ILIVYOELEKEZWA NA RAIS

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS**
**INNOCENT BASHUNGWA**



# RAIS SAMIA:
# SENSA
## NI YA KILA MTANZANIA



**Ukuaji wa shughuli za kitakwimu kunaenda sanjari na mahitaji ya majengo ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikiwemo Ofisi za Mikoa pamoja na vitendea kazi kama magari na vinginevyo.**

ILI iwe rahisi kwa serikali kupanga mipango ya maendeleo ya nchi na wananchi wake ni lazima ijue idadi ya watu ilio nao. Nchi isiyojua idadi ya watu wake haiwezi kufikisha maendeleo kwa haraka kwa wananchi.

Ukweli wa jambo hilo umemfanya Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kuwaagiza viongozi kutoa elimu na mafunzo kwa wananchi wote ili wajitokeze na kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, 2022.

Alitoa agizo hilo Aprili 8,2022 wakati wa uzinduzi wa nembo na tarehe ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika Hoteli ya Golden Tulip, Unguja visiwani Zanzibar.

Rais alieleza sensa ni ya kila mtu una ili ifanikiwe, uelimishaji na uhamasishaji ni masuala yanayotakiwa kupewa kipaumbele kuwasaidia wananchi kutoa taarifa kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi zitakazoiwezesha kupanga mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Rais Samia pia, alisisitiza elimu hiyo kutokana na changamoto za baadhi ya mila, desturi na imani potofu kwa baadhi ya jamii ambazo zinachukulia kuhesabiwa au kutaja idadi ya watoto au wanakaya waliopo ni kukaribisha laana na mkosi.

Vile vile, Rais Samia alieeleza mwenendo wa baadhi ya jamii au familia kuwaficha na kuwazuia watu wenye ulemavu kutoshiriki katika kuhesabiwa ni kinyume na haki za binadamu.

Tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanzania, tayari zimefanyika Sensa nyingine tano katika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.





**Baada ya miaka**
**10**
**hatimaye mwaka huu Tanzania itafanya sensa ya watu na makazi**



# SENSA
## YA MAJENGO MUHIMU KWA
# TAIFA

## SENSA YA MAJENGO

# 2022

**Sensa ya mwaka huu pia itahusisha majengo kama inavyoeleza Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 katika ibara ya 4.1.8.2(ii) inaelekeza wizara kuwa na benki ya taarifa za makazi na nyumba ili kusaidia katika maamuzi mbalimbali ya maboresho ya kisekta kwa kujua hali ya makazi,**




**Ukuaji wa shughuli za kitakwimu kunaenda sanjari na mahitaji ya majengo ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikiwemo Ofisi za Mikoa pamoja na vitendea kazi kama magari na vinginevyo.**

BAADA ya miaka 10 hatimaye mwaka huu Tanzania itafanya sensa ya watu na makazi, zoezi hili ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Sensa ya mwaka huu pia itahusisha majengo kama inavyoeleza Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 katika ibara ya 4.1.8.2(ii) inaelekeza wizara kuwa na benki ya taarifa za makazi na nyumba ili kusaidia katika maamuzi mbalimbali ya maboresho ya kisekta kwa kujua hali ya makazi, ukuaji wa miji, vifaa vya ujenzi, ujenzi wa nyumba kupitia ushirika, tozo za kodi ya pango la jengo, gharama za ujenzi wa nyumba, mchango wa sekta binafsi katika nyumba, mchango wa serikali katika nyumba na mahitaji ya nyumba.

Aidha, utekelezaji wa Sensa ya majengo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020/2025, ibara 76(d) ambayo imeelekeza Wizara kutambua na kuandaa kanzidata ya nyumba zote nchini kwa kushirikiana na wadau pamoja na kuimarisha mahusiano kati ya wapangaji na wenye nyumba.

# SENSA
YA MAJENGO

**01** KUPATA TAKWIMU ZA MAJENGO ZENYE UHAKIKA NA KUWA NA KANZIDATA YA TAIFA YA TAARIFA ZA MAJENGO.

**02** KUSAIDIA KATIKA UANDAAJI WA SERA, SHERIA, KANUNI NA PROGRAM MBALIMBALI ZA MABORESHO YA SEKTA YA NYUMBA NCHINI.

**03** KUWEZESHA SERIKALI KUPATA TAARIFA ZA MATUMIZI YA MAJENGO KAMA UPANGISHAJI WA NYUMBA, BIASHARA NA HUDUMA ZA JAMII.

**04** KUIWEZESHA SERIKALI KUJUA MCHANGO WAKE KATIKA UPATIKANAJI WA NYUMBA ZA MAKAZI NCHINI KAMA INAVYOOELEKEZWA KWENYE IBARA YA 4.2.2 YA SERA YA MAENDELEO YA MAKAZI.

**05** .KUIWEZESHA SERIKALI KUFANYA TATHMINI YA KIWANGO CHA NYUMBA ZILIZOJENGWA MAENEO YALIYOPANGWA NA YASIYOPANGWA NA HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA JAMII KATIKA MAJENGO.

**06** KUIWEZESHA SERIKALI KUTAMBUA HALI YA UENDELEZAJI WA MIJI KWA UJENZI WA KAWAIDA AU MAGHOROFA NA KUJUA AINA ZA MAJENGO YALIYOJENGWA NCHINI.

**07** KUWEZESHA UTOAJI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU YA KIMATAIFA SDG LENGO NAMBA 11 NA AGENDA 2030 LILILOTOLEWA NA SHIRIKA LA MAKAZI DUNIANI LINALOTOKANA NA MAENDELEO YA MAKAZI YALIYOJUMUISHA USALAMA, USTAHIMILIVU NA UENDELEVU.

**08** KUSAIDIA KATIKA TAFITI ZA MASUALA YA NYUMBA NA MAJENGO.



AINA ZA
# MAJENGO YATAKAYOHESABIWA



JENGO LA PEKE YAKE (DETACHED BUILDING)



.NYUMBA MBILI ZILIZOUNGANA (SEMI DETACHED BUILDING)



SAFU ZA MAJENGO (ROW HAUSES).

## CHANGAMOTO

Pamoja na umuhimu wa sensa ya majengo, lakini kumekuwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa watu wa kutoa taarifa za majengo hasa kwenye majengo yaliyohamwa, majengo ambayo wamiliki wamesafiri, taasisi, majengo ambayo ujenzi unaendelea na yaliyopangishwa.

Hata hivyo yapo mapendekezo kadhaa yaliyotolewa katika kukabiliana na changamoto hizo ambazo ni kuelimisha jamii na kuongeza kasi ya uhamasishaji kwa wananchi. Wananchi waelekezwe kuacha taarifa za majengo hususan majina kamili ya mmiliki, namba za simu, nakala ya hati au barua ya toleo au hati ya kukiri malipo kwa maeneo yote yaliyopangwa na kupimwa.

Wamiliki wa majengo ambayo hayajakamilika kujaza fomu maalum ya taarifa za majengo yao na kuziacha kwa viongozi wa mitaa au vitongoji. Muhimu ni kutambua kuwa sensa ni mahususi kwa maendeleo ya Taifa.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# ENROLL
# TWIGA MILES

AND GET **1,000** AWARD POINTS




www.airtanzania.co.tz

airtanzania_atcl

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

# SENSA

## KUISAIDIA SERIKALI YA RAIS SAMIA

SENSA YA WATU NA MAKAZI NI ZOEZI LA KITAIFA LINALOFANYIKA KILA BAADA YA MIAKA 10



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kufanya Sensa ya Watu na Makazi ifikapo mwezi Agosti mwaka huu. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), ipo kwenye maandalizi ya kufanya Sensa hiyo.

Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi la kitaifa linalofanyika kila baada ya miaka 10 ambapo Sensa ya mwisho kufanyika nchini ni ile ya mwaka 2012. Hivyo Sensa ya mwaka 2022 itakuwa ni sensa ya Sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

## MAANA YA SENSA YA WATU NA MAKAZI

Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum. Kwa maana nyingine, sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi. Takwimu hizi za msingi ndiyo zinazoweza kuanisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

**Sensa ya mwaka 2022 itakuwa ni sensa ya Sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964**



# UMUHIMU WA SENSA 2022

Kuisadia Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa;

Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;

Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;

Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano Pato la mtu mmoja mmoja, Pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;

Taarifa itakayowezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira; na

Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia. Takwimu sahihi za Sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

## MADODOSO YA SENSA

Sensa ya mwaka 2022 kama zilivyo sensa zilizopita itatumia aina mbili kuu za madodoso. Dodoso



refu litakalotumika kuhoji asilimia 30 ya maeneo yote ya kuhesabia watu na Dodoso fupi litakalotumika kuhoji kwenye asilimia 70 ya maeneo yote ya kuhesabia watu.
Madodoso Mengine ni:-

Dodoso la Taasisi ambalo ni mahsusi kwa ajili ya wasafiri, waliolala mahotelini/nyumba za wageni, na waliolazwa hospitalini; na

Dodoso la Wasio na Makazi maalum ambalo ni mahsusi kwa watu wote wanaolala maeneo yasiyo rasmi, kwenye baraza za majengo mbalimbali, kwenye madaraja na maeneo mengine.

## MAANDALIZI 2022

Utekelezaji wa sensa ya watu na makazi hufanyika katika awamu kuu tatu kuu ambazo ni Kipindi Kabla ya Kuhesabu Watu, Wakati wa Kuhesabu Watu na Kipindi Baada ya Kuhesabu Watu.
Kipindi Kabla ya Kuhesabu Watu
Kipindi kabla ya kuhesabu watu kinajumuisha Uandaaji wa Kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa na nyaraka nyingine, Utengaji wa Maeneo ya Kuhesabia Watu na Uzalishaji wa Ramani, Uandaaji wa Nyenzo (Madodoso na Miongozo mbalimbali); Uhamasishaji, Sensa ya Majaribio ifikapo tarehe 29 Agosti 2021 ikiwa ni mwaka mmoja kamili kabla ya Sensa yenyewe; Kuunda kamati za sensa; kufanya mikutano na wadau wa takwimu; kufanya manunuzi, kufanya uchaguzi wa aina ya teknolojia itakayotumika, kuajiri wadadisi na wasimamizi, usambazaji wa vifaa; na kufanya maandalizi ya Tathmini ya Sensa.

## KIPINDI CHA KUHESABU WATU

Kipindi cha kuhesabu watu kinajumuisha kazi kuu na ya muhimu katika zoezi hili ya kuhesabu watu.

## BAADA YA KUHESABU WATU

Kipindi baada ya kuhesabu watu kinajumuisha Uchakataji wa Taarifa za Sensa, Uchambuzi, Utoaji wa Matokeo ya Awali, Usambazaji wa matokeo ya mwisho, uhamasishaji wa matumizi ya takwimu kwa watumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Maandalizi ya sensa ya watu na makazi 2022 yalianza 2018, ikiwa ni kutenga maeneo ya kuhesabia watu, kutayarisha nyaraka muhimu za sensa kama vile madodoso, miongozo, fomu za kudhibiti ubora na kufanya sensa ya majaribio.

Kwa sasa maandalizi ya sensa yamefikia katika hatua zifuatazo;

1. Kuandaa Kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022;

2. Kutenga Maeneo katika wilaya 5 za mkoa wa Dodoma ambazo ni Bahi, Chamwino, Kondoa, na Chemba; na Wilaya moja ya Mkoa wa Singida (Singida Mjini);

3. Kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu inaendelea katika mkoa wa Singida katika wilaya za Manyoni, Ikungi; na mkoani Dodoma katika wilaya za Mpwapwa na Kongwa.

4. Kufanyika kwa ziara moja ya kimafunzo nchini Kenya kwa ufadhili wa UNFPA ambao wamefanya sensa ya kidigitali hivi karibuni na kujifunza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kufanya sensa kwa mafanikio. Matumizi ya teknolojia hii itasaidia kupunguza gharama za kufanya sensa na kupunguza muda wa kutoa matokeo ya sensa.
5. Kuandaa rasimu ya Dodoso la Sensa na nyaraka nyingine muhimu kama vile miongozo ya kufundishia, miongozo ya makarani wa sensa, miongozo ya wasimamizi wa sensa na miongozo ya waratibu wa sensa mkoa na wilaya.

## MASWALI MUHIMU

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ina moduli kumi na nne ambazo zitatumika kukusanya taarifa za watu na makazi yao nchi nzima.

**Maswali yatakayoulizwa yatahusu:-**

1. Taarifa za kidemografia (umri, jinsi, uhusiano, hali ya ndoa, uraia, n.k.);
2. Maswali yanayohusu ulemavu;
3. Taarifa za Elimu;
4. Maswali ya uhamaji, pamoja na taarifa za Watanzania wanaoishi nje ya nchi
5. Maswali kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (vitambulisho vya NIDA, Mzanzibari mkazi, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva)
6. Shughuli za kiuchumi
7. Umiliki wa ardhi na taarifa za TEHAMA





## TOFAUTI YA SENSA YA 2022 NA ZILIZOPITA:-

Katika sensa ya mwaka 2022 inatarajiwa kuwa na vitu vipya kama vile;
Kutenga maeneo ya kijiografia ya kuhesabia watu katika ngazi za kitongoji/mtaa na upatikanaji wa taarifa za kitakwimu katika ngazi za kitongoji/mtaa pamoja na kuwa na mipaka ya kudumu katika ngazi hizo;

Matumizi ya Vishikwambi (tablets) katika hatua zote za utekelezaji wa sensa kwa lengo la kupunguza gharama;

Nyongeza ya maswali yatakayowezesha upatikanaji wa taarifa zaidi za kitakwimu ikilinganishwa na Sensa ya Mwaka 2012:-

1. Taarifa za kidemografia (umri wakati wa ndoa ya kwanza);

2. Maswali yanayohusu ulemavu (Kichwa kikubwa, Mgongo wazi, Kifafa/ Epilepsy, Mbalanga/storiasis na Usonji/autism);

3. Maswali ya uhamaji kulingana na mapendekezo ya IOM (International Organization of Migration);

4. Maswali kuhusu umiliki wa nyaraka za kitaifa (vitambulisho NIDA, vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo wadogo, Mzanzibari mkazi, hati ya kusafiria, na leseni ya udereva);

5. Maboresho ya maswali ya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na idadi ya kaya ziliko kwenye sekta isiyo rasmi;

6. Umiliki wa ardhi na taarifa za TEHAMA

- Takwimu za nyumba (orodha, hali ya umiliki na aina ya nyumba)
- Maswali ya kilimo na mifugo

Matarajio ya Ofisi ni kujipanga vizuri kwa kutumia rasilimali chache zilizopo ili kukamilisha kwa wakati shughuli zote za maandalizi ikiwamo:-

1. Kazi ya utengaji wa Maeneo ya Kuhesabia Watu katika ngazi ya kitongoji na mtaa ambayo ndiyo msingi wa kufanikisha sensa kwa ubora

2. Uandaaji wa nyaraka za sensa;

3. Uundaji wa vikosi kazi/units kwa lengo la kugawana majukumu; na

4. Ufanyaji wa Sensa ya majaribio tarehe 29 Agosti 2021



Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

# MUFTI:

## TUSHIRIKI ZOEZI LA

# SENSA





Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubeir bin Ally amewataka Waislamu nchini kuunga mkono na kushiriki katika Sensa ya wat una makazi ifikapo Agosti 23 mwaka huu.

Ametoa kauli hiyo kwenye Swala ya Ijumaa katika Msikiti Mkuu wa BAKWATA wa Mohamed VI Kinondoni Muslim, jijini Dar es salaam.

## UMUHIMU

Je, wajua kwamba ili Serikali iweze kuwahudumia wananchi wake ipasavyo inatumia takwimu zitokanazo na Sensa ya Watu na Makazi? Jiandae Kuhesabiwa! Na shiriki kikamilifu #SensaTZ2022

**ili Serikali iweze kuwahudumia wananchi wake ipasavyo inatumia takwimu zitokanazo na Sensa ya Watu na Makazi? Jiandae Kuhesabiwa! Na shiriki kikamilifu**



## SHEIKH PONDA:

# SENSA

## NI MUHIMU KWA TAIFA

NA YUSUPH KATIMBA

SHEIKH Ponda Issa Ponda, Katibu wa Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania ni miongoni mwa viongozi wa dini wenye kariba ya aina yake. Wanaheshimika, kusikilizwa na kuthaminika katika jamii.

Idadi kubwa ya waumini wa dini ya Kiislamu na hata baadhi ya waumini wa madhehebu mengine, wanamtazama kama msemaji na mtetezi wa kweli wa waislamu na uislamu kwa ujumla.

Dhamira yake hiyo ya kutetea uislamu na kuwatetea waislamu ilimsababishia kukumbana na misukosuko kadha wa kadha ikiwa ni pamoja na kutuhumiwa makosa ya uchochezi yaliyomsababishia kukamatwa na kuwekwa ndani mara kadhaa.

Katika kuendeleza harakati zake za utetezi, Sheikh Ponda alishawahi kuingia kwenye sintofahamu baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa takwimu za idadi ya waislamu mwaka 2012.

Hakuwa akikubaliana na takwimu zilizokuwa zikitolewa wakati huo na baadhi ya madhehebu ya dini kuwa, wakristo ni wengi kuliko waislamu.

Hatua yake hiyo ilidaiwa kuzalisha changamoto kwenye zoezi la Sensa la mwaka 2012. Hata hivyo kwa sasa Sheikh Ponda ana mtazamo tofauti juu ya umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi katika nchi.

Anajua wazi kuwa sensa ina umuhimu kwa nchi, hatua yake hiyo inaongeza hamasa kwa Wananchi kushiriki kwa kuwa, anaamini taifa bila kuwa na taarifa za msingi, haliwezi kusonga mbele.

Kiongozi huyo wa kidini amesema, serikali yoyote duniani isipofanya Sensa ya Watu na Makazi, kamwe haitajua mahitaji yake halisi na serikali hiyo itafeli kuhudumia taifa lake.

**Sensa ni muhimu sana, serikali inakuwa katika mazingira mazuri ya kuhudumia nchi na wananchi kwa ujumla**

# SHEIKH PONDA
## sensa ni muhimu kwa taifa

Katika mahojiano maalumu na jarida hili, Sheikh Ponda amesema, Sensa ni muhimu kwa kuwa ndio msingi wa kupanga maendeleo katika nchi.
Yafuatayo ni mahojiano hayo:-

**TZ&BEYOND:** Sheikh Ponda, nchi inaelekea kwenye zoezi la kufanya sensa ya watu na makazi, kuna umuhimu wowote kwenye zoezi hili?
**SHEIKH PONDA:** Sensa ni muhimu sana, serikali inakuwa katika mazingira mazuri ya kuhudumia nchi na wananchi kwa ujumla, serikali inakuwa na taarifa zote muhimu. Hakuna serikali inayoendeshwa duniani bila kujua mahitaji yake muhimu. Sensa haiepukiki.

**TZ& BEYOND:** Wananchi wangependa kujua umuhimu wa Sensa na Makazi?
**SHEIKH PONDA:** Sensa husaidia kuonesha picha halisi ya nchi, huisadia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo iliyowekwa, husaidia kupanga huduma za afya na pia ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.

Sensa hugusa takwimu za viumbe wote sambamba na kuwepo kwa mipango katika ngazi zote. Na kwamba, taarifa zinazotokana na sensa, husaidia serikali kujua ongezeko la idadi ya watu na usimamizi wa mazingira.

**TZ&BEYOND:** Kwenye zoezi la Sensa la mwaka 2012 kuliibuka sintofahamu na taasisi yako ilihusishwa na madai ya kukwamisha zoezi hilo, unaweza kulizungumzia hili?

**SHEIKH PONDA:** Taasisi yetu ilipata mshtuko baada ya kuwepo kwa takwimu za kupikwa kuhusu kipengele cha idadi ya waumini wa dini kwenye baadhi ya taarifa za vyombo vya habari, serikali na mitandao ya taasisi za kidini.

Kabla ya mabadiliko yaliyofanywa na Mwalimu Julius Nyerere ya kuondoa kipengele cha dini katika Sensa, kipengele hicho kilikuwepo kuanzia wakati wa utawala wa Mjerumani hadi Muingereza.

Kipengele hicho kilikuwepo mpaka Sensa ya mwisho wakati wa ukoloni mwaka 1957. Sensa iliyofuata baada ya uhuru, iliondoa kipengele hicho.

Baada ya kuondolewa kipengele hicho, takwimu tofauti tofauti zilianza kutolewa na mashirika ya dini, vyombo vya habari vikaanza kutumia takwimu hizo na katika baadhi ya maeneo serikali nayo ikaanza kutumia takwimu hizo.



**Sensa husaidia kuonesha picha halisi ya nchi**





# SHEIKH PONDA
# sensa ni muhimu kwa Taifa

Kwa vyombo vya habari pamoja na serikali haikuwa sahihi kutumia takwimu zilizotolewa na taasisi za dini kwani taasisi hizo zilipaswa kuwa na takwimu za waumini wao tu. Serikali iliacha kutumia kipengele hicho, tukawa tunajiuliza Waislam wanawezaje kutoa takwimu za waumini wa madhehebu mengine wakati hawawafanyii Sensa! Tukajiridhisha kuwa takwimu zinazotolewa na taasisi za dini zinakuwa si sahihi na ndio tukaona umuhimu wa kuridisha kipengele hicho.

**TZ&BEYOND:** Mlitumia njia gani kufikisha malalamiko yenu?
**SHAIKH PONDA:** Taasisi yetu iliandika barua kwenda serikalini, tulitaka kipengele hicho kirejeshwe ili taarifa za takwimu zinazotolewa ziwe za serikali na zenye kuaminika.

Juni 11, 2012 tulialikwa kwenye kikao na taasisi iliyokuwa ikiratibu zoezi la Sensa, kwenye kikao hicho tulialikwa madhehebu ya dini pamoja na viongozi wengine wa serikali.

Tulieleza kilichotokea na kufafanua umuhimu wa kuingiza kipengele cha dini ili kupata takwimu halisi za kitaifa na zisizo za upotoshaji.

Hoja zetu zilikuwa ni pamoja na kuzuia upikwaji wa tawimu kama ilivyoanza kujitokeza kwa taasisi binafsi, pia ni hitaji la dunia kwa maana nchi zote zimekuwa na kipengele hicho. Mfano Uingereza, Ujerumani, Saudi Arabia, Senegal, Uganda na nchi nyingine duniani. Serikali haikuwa tayari kukubaliana na hoja hizo na baadaye msimamo wa kugomea Sensa ulikuwa na athari kubwa wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo mwaka 2012.

**TZ&BEYOND:** Nini kilitokea baada ya kugomea?
**SHEIKH PONDA:** Watu walikamatwa lakini kubwa zaidi yaliibuka maandamano makubwa tarehe Septemba 6,2012 yaliyoelekea Wizara ya Mambo ya Ndani, Posta jijini Dar es Salaam. Serikali ililazimika kuongeza muda wa Sensa kutokana na vikwazo vya watu kuhesabiwa.
**TZ&BEYOND:** Kuna mabadiliko yeyote kwenye Sensa ya mwaka huu?

**SHEIKH PONDA:** Serikali imetangaza kutokuwepo kwa kipengele cha dini, lakini naamini katika siku zijazo, kipengele hicho kitarejeshwa.

Nirudie, Sensa ni muhimu sana kwa nchi. Hatuwezi kwenda mbele bila kufanya Sensa na kujua mahitaji yetu. Hivyo, Sensa haiepukiki. Hata kama kipengele cha dini hakimo, mbele ya safari serikali itaona umuhimu wa kukiweka kama ilivyo kwa serikali zingine duniani.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti 2022. Hii ni Sensa ya Sita kufanyika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1964, sensa zilizotangulia zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Serikali inafanya hivyo kutokana na umuhimu wake, lakini pia ni hitajio la dunia kwa maana ya kila nchi huhitaji kujua idadi ya watu wake, mifugo na mwisho hutambua mahitaji halisi ya nchi.

Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), ndio inayoratibu Sensa kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura 351.

Uzinduzi huu wa Sensa 2022, ulifanyika tarehe 22 Mei 2021 katika Viwanja vya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, jijini Dodoma.

Tofauti na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, ambayo iliingia dosari kwa watu kugoma kuhesabiwa, Sensa ya Mwaka 2022 haina kikwazo chochote. TUJIANDAE KUHESABIWA.







**Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya Sensa ya Watu na Makazi tarehe**

**23**

**Agosti**

Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

# RAIS DK. HUSSEIN

## 'idadi yetu mtaji wetu'

**Rais Dkt. Mwinyi aliyasema hayo Aprili 8, 2022 kwenye uzinduzi rasmi wa nembo ya sensa pamoja na tarehe ya kuhesabiwa ambayo ni Agosti 23**

KWA mara ya sita Tanzania inarejea tena kwenye zoezi la kuhesabiwa ambalo linajulikana kama sensa ya wat una makazi.

Kwa mara ya kwanza tangu Tanganyika na baadae Tanzania kupata uhuru watu wake walihesabiwa mwaka 1967, ikumbukwe kuwa kabla ya uhuru zoezi hilo pia lilikuwepo, hata hivyo lilikuwa likifanywa na wakoloni kwa kuhusisha nchi zote za Afrika Mashariki.

Baada ya zoezi la 1967, kukamilika Tanzania ilifanya tena sensa mwaka 1978, 1988, 2002 na sensa ya mwisho ilikuwa ni mwaka 2012.

Kifupi zoezi la sensa hufanyika kila baada ya miaka 10, kwenye zoezi la mwaka huu, muitikio wa watu kuhesabiwa umekuwa ni mkubwa na hasa ikizingatiwa kuwa serekali haiwezi kuandaa ama kutekeleza mipango endelevu pasi kujua idadi ya watu.

Ukweli huo umemuibua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kubainisha kuwa idadi yetu ndio mtaji wetu.

Rais Dkt. Mwinyi aliyasema hayo Aprili 8, 2022 kwenye uzinduzi rasmi wa nembo ya sensa pamoja na tarehe ya kuhesabiwa ambayo ni Agosti 23, 2022.

Katika hotuba yake uzinduzi rasmi wa matumizi ya nembo na tarehe ya sensa, uliofanyika Unguja visiwani Zanzibar, Rais Dkt. Mwinyi aliwashukuru viongozi wa kamati ya sensa, inayoongozwa na Mwenyeviti ambaye pia ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Menyekiti mwenza, ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalah kwa kazi nzuri waliyoifanya.

"Wamekuwa na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi, viongozi hao wamekuwa na utaratibu wa kuwatembelea viongozi wa juu ili kushauriana na kupokea ushauri muhimu.

"Naipongeza kamati kwa kukamilisha sensa ya majaribio kwa ufanisi mkubwa, naamini mafanikio yaliyopatikana katika sensa ya majiribio iliyofanywa katika mikoa 18 ikiwemo mikoa yote mitano ya Zanzibar pamoja na changamoto zilizojitokeza yatakuwa ni dira ya kufanikisha kwa ufanisi kazi iliyobaki.




RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, DKT. HUSSEIN ALI MWINYI



**Naipongeza kamati kwa kukamilisha sensa ya majaribio kwa ufanisi mkubwa, naamini mafanikio yaliyopatikana katika sensa ya majiribio iliyofanywa katika mikoa**

# 18

"Uzinduzi huu wa nembo ya sensa ambao umebeba kauli mbiu pamoja na tarehe ya sensa ni muhimu katika kufanikisha zoezi hilo, ujumbe uliobebwa kwenye nembo unatutaka tujitayarishe kushiriki na kufanikisha zoezi hilo na ujumbe huo unatufahamisha lini zoezi hilo litafanyika, ni ujumbe muhimu unawasilishwa kwetu kwa njia fupi na sahihi kwa kutumia Sanaa.

"Naamini kuanzia leo wananchi hawatauliza ni lini zoezi hilo litafanyika ila tutaendeleza kazi ya kuhamasishana. Tuzingatie kwamba idadi yetu ni mtaji wetu, tunapaswa tuijue ili tuitumie vizuri.

"Naungana nawe katika kuwahimiza wananchi tuunge mkono juhudu zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zote mbili katika kuhakikisha tunafanikisha vizuri zoezi hili la sensa na makazi.

"Sote tunapaswa kuzingatia kuwa upangaji na utekelzaji wa mipango yetu ya maendeleo, unahitaji kufanywa kwa kutumia takwimu za idadi ya watu zinazopatikana kupitia sensa kutoka ngazi ya shehia, jimbo, wilaya, mkoa hadi taifa.

Serikali zetu zinahitaji kujua idadi ya watu katika kila familia na maeneo ya utawala ili kuweza kuimarisha utoaji wa huduma za jamii na ujenzi wa miundo mbinu.

Aidha utekelezaji wa dhamira yetu ya kuendesha uchumi kwa njia za kidigitali unahitaji kuwa na takwimu sahihi za watu, makazi yao pamoja na shughuli wanazozifanya, utumiaji wa takwimu sahihi kwa kutumia teknolojia ya kisasa utarahisha utekelezaji wa mipango yetu katika ukusanyaji wa mapato kuwa na mifumo jumuishi ya kifedha, mifumo bora ya bima ya afya, pamoja na mifumo imara ya mawasiliano kwa njia ya sim una mitandao.

Nawahimiza wataalamu na viongozi wa umma na sekta binafsi kuongeza kasi ya matumizi ya takwimu katika kupanga na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo yetu.



# Dk. Mwigulu atoa *Wito...*



**Katika mkutano huu serikali imejumuisha asasi za kiraia na sekta binafsi ili zipate taarifa za maendeleo na fursa ya kuona namna ya kushiriki katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi**

SERIKALI imetoa wito kwa washirika wa maendeleo kuiunga mkono katika kufanikisha ufanyikaji wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati akifungua mkutano wa majadiliano ya kimkakati wa ngazi za juu uliohusisha mawaziri, mabalozi, sekta binafsi na asasi za kiraia, jijini Dar es Salaam.

"Sensa ya Watu na Makazi itaiwezesha serikali kupata takwimu sahihi, kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo, mageuzi ya sekta za kijamii na kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza mipango na kugawa rasilimali kulingana na mahitaji," alisema.

Hata hivyo, amesema wapo baadhi ya washirika wa maendeleo walioanza kuchangia ili kufanikisha sensa hiyo na kuwasisitiza wengine kuendelea kufanya hivyo.

Amesema kuwa mkutano huo umehusisha sekta binafsi na asasi za kiraia kwa kuwa ni wadau muhimu katika maendeleo na kwamba serikali inaweka mazingira wezeshi ili kukua na kutengeneza ajira nchini na kukuza kipato cha wananchi na uchumi.

"Katika mkutano huu serikali imejumuisha asasi za kiraia na sekta binafsi ili zipate taarifa za maendeleo na fursa ya kuona namna ya kushiriki katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi," alisema.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kassim Ali, alisema mkutano huo umetoa fursa ya nchi kukutana na washirika wa maendeleo na kuwasilisha mipango iliyopangwa ili kuona namna ya kushiriki.

Akizungumza kwa niaba ya Washirika wa maendeleo Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donnell, alisema kwa muda mrefu wamewekeza mabilioni ya fedha kwa ajili ya kuchangia maendeleo endelevu ya nchi na kwamba wapo tayari muda wote.

Alisema washirika wa maendeleo wataendelea kufanya hivyo katika masuala ya elimu, mazingira, afya na utawala bora na wanaamini kuwa fedha hizo zitatumika kama ilivyokusudiwa.

Balozi O'Donnell alipendekeza mambo manne kutiliwa mkazo ikiwemo usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi, demokrasia, utawala bora na haki za binadamu.

Alisema mambo hayo ni muhimu kwa amani, maendeleo na jamii endelevu, kuweka mpango mzuri wa kupata nishati, kuhifadhi mazingira na uchumi wa bluu ambavyo visipofanyiwa kazi vina madhara katika maendeleo.



# DK. MALASUSA: SENSA NI HITAJI LA MUNGU

# Q&A

MWAKA huu wa 2022, Tanzania itafanya zoezi la Sensa ambalo mara ya mwisho lilifanyika nchini mwaka 2012, ambapo Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni 40.

Hatua hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake, hasa ikizingatiwa kuwa familia inayojua idadi ya watu wake inajirahisishia namna ya kupanga mipango yake.

Kutokana na umuhimu huo Jarida hili liliona haja ya kufanya mazungumzo na wadau wakuu wa sensa ambayo inatajwa kutambulika hata kwenye vitabu vya dini zote duniani ukiwamo ukristo na uislamu.

Ikumbukwe kuwa pamoja na kuwapo kwa imani mbalimbali za dini, lakini ukweli ni kwamba kwa Tanzania dini zenye nguvu ni ukristo na uislamu.

Miongoni mwa wadau hao ni Baba Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, ambaye pia ni mlezi wa Kamati ya amani na Kamati ya Maridhiano Dk. Alex Malasusa.

Katika mahojiano haya Askofu Dk. Malasusa alizungumzia umuhimu wa sensa mbele za Mungu pamoja na utii kwa viongozi waliopewa dhama ya kuliongoza taifa hili.

**TZ&BEYOND:** Wewe ni kiongozi wa dini na msomi, unaizungumziaje Sensa ya watu na Makazi ambayo itafanyika Agosti 23, 2022?

**ASKOFU MALASUSA:** Sensa ya watu na makazi ni muhimu sana kwa taifa letu, taifa ambalo halijui idadi ya watu wake ni taifa lililokufa.

Taifa hilo litakuwa haliwezi kupanga mipango yake, haliwezi kujua idadi ya makazi yaliyopo ndani ya nchi, haliwezi kujua hata kiwango cha kuishi cha watu wake.Kazi ya kuhesabiwa ni kazi ya kimungu, kazi hii ya Sensa ni kazi ambayo ipo kwenye Kuraan na hata kwenye Biblia, nasisitiza kazi hii ni ya kimungu.

**TZ&BEYOND:** Kama ni kazi ya kimungu iweje sasa ifanywe na binadamu?

**ASKOFU MALASUSA**: Nikwambie hata Mungu mwenyewe alitamani na alipenda kujua idadi ya watu wake, si kwamba yeye hakuwezi kuwahesabu, kwa heshima yake na upendo wake, aliamua kutushirikisha na kutupa heshima wanadamu kuifanya kazi yake, kazi ambayo ingeweza kufanywa na malaika.

Kuna wakati Mungu alitamani kujua idadi ya watu wake na akamwambia Daudi afanye kazi hiyo nae akaifanya kwa kuwakahesabu watu. Sensa si jambo la mchezo.

TZ&BEYOND: Unadhani Sensa ya mwaka huu itakuwa na tofauti na zile zilizopita?

ASKOFU MALASUSA: Naamini hivyo, na ningetamani Sensa ya mwaka huu iwe tofauti kabisa na miaka yote iliyopita, kwa sababu kimsingi kazi hii ni kazi yetu viongozi wa dini.

Sisi viongozi wa dini ndio tunatamani wananchi ambao ni waamini wetu wapate vituo vya afya, shule na mahitaji mengine mengi, kitendo cha kujua idadi yao kitasaidia kufikisha kwa haraka huduma hizo kwa kushirikiana na serikali.

Viongozi wa dini ndio tuko mstari wa mbele kufanya kazi hiyo, tuseme wazi kuwa sisi ndio tunasaidiwa na serikali ambayo yenyewe inasema sisi ni wadau na tunafanya kazi pamoja, lakini sisi ndio tunasaidiwa na serikali.

Natamani katika Misikiti yetu, katika Makanisa yetu na katika Mahekalu yetu,tuisemee sensa, tuwaeleze waumini wetu wawe tayari kuhesabiwa, tuwaambie wale watakaokutwa kwenye maeneo yao awe mkuu wa kaya au kaimu mkuuu wa kaya akubali kuhesbiwa.

**TZ&BEYOND:** Wapo wanaoamini kuwa kitendo cha kuhesabiwa kina dhamira ya kutaka kupunguza idadi ya watu, umeshawahi kulisikia hili na unalizungumziaje?

**ASKOFU MALASUSA:**

Nimelisikia hilo, niseme wazi Sensa haina jambo lolote la hila, sensa ipo kwenye Biblia na ipo kwenye Kuraan, ni jambo ambalo Mungu

ameliruhusu na taifa letu mwaka huu tutapata baraka hiyo.

UTII

**TZ&BEYOND:** Unadhani ni kwanini wapo wanaodhani sensa ina hila ndani yake?

**ASKOFU MALASUSA:** Shida kubwa ya mwanadamu ni kutii, mwanadamu anaweza kusema mambo mengi lakini akakosa utii na Mungu hapendezwi na mwanadamu asiye tii.

Kutii ni jambo tofauti sana, sifa moja ya kiumbe kilichoumbwa na Mungu yaani mwanadamu ni utii. Mungu alitamani mwanadamu awe na utii, hata Kuraan imejaa masuala ya utii na hii ndio raha ya Tanzania, waislamu na wakristo wanaweza kukumbushana, ukimkuta Muislamu au Mkristo hana utii basi ujue hiyo ni tabia yake na si dini yake.

Mungu anataka sisi sote tuwe watii na alituumba ili tumtii yeye, katika biblia vitabu vyote kutoka Mwanzo hadi Ufunio vinahimiza sana mwanadamu kuwa mtii.

Katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati, Mungu ameweka amri 10 ili mwanadamu akizitimiza hizo apite katika dunia hii kwa furaha, aone mema ya nchi, tena anajumlisha katika sura ya 11 kwa maneno mafupi sana, anasema 'Tii utabarikiwe'.

Sensa hii ambayo tunakwenda kuifanya kama sisi viongozi wa dini na wafuasi tutatii haya ambayo tumeelezwa, nchi yetu itabarikiwa sana, tutajua wapi hakuna shule, hakuna vituo vya afya, wapi tuanzishe jambo hili na lile, wapi kuna utapiamlo, ukweli ni kwamba kila sekta itazitumia takwimu hizi.

Tii utabarikiwa, tii utaishi, nina uhakika viongozi wa dini na wafuasi wao wakilifuata hili la utii nchi yetu itakwenda kupiga hatua kubwa sana. Ikumbukwe utii si kusikia tu, bali ni kutekeleza ulichoambiwa.

Kibiblia utii ni kuonesha upendo kwa Mungu aliyekuumba, natamani kuliendeleza hili la kutii mamlaka zilizowekwa, Tanzania tumekuwa watii sana kwa mamlaka zilizowekwa ingawa wapo wachache wasio tii.

Yesu aliwahi kusema kama unanipenda, utazishika amri zangu, huwezi kusema nakupenda Yesu wakati huzishiki amri zangu. Kutii si kwa ajili ya mambo unayoyapenda tu, hata kwa yale yanayokuudhi.

**TZ&BEYOND:** Unawashauri nini viongozi wenzako wa dini?

**ASKOFU MALASUSA:** Yesu alikuwa mtii hata katika mauti, alitii mauti ya msalaba na katika hili la Sensa hata sisi viongozi wa dini tunapaswa kuwa watii.

Hili suala ni letu, serikali inatusaidia, nawaomba viongozi wa dini waliseme hili la Sensa mara kwa mara.

Tukubaliane utii si ujinga, woga ama kuonesha huna nguvu, utii ni hekima ya kimungu, sensa ni jambo ambalo Mungu ameliruhusu, sensa ni jambo la kimaendeleo, sensa itaboresha maisha yetu na sensa itarahisisha mipango ya maendeleo, sensa itatupa neema katika nchi yetu.

Neno la mungu linesema 'Wa heri wanaosikia neno la Mungu na kulifanyia kazi,' heri sisi ambao tumapata nafasi ya kusikia habari hii na kwenda kuifanyia kazi.

Niwaombe watanzania wote wawe tayari kuhesabiwa siku hiyo.

**Hatua hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake, hasa ikizingatiwa kuwa familia inayojua idadi ya watu wake inajirahisishia namna ya kupanga mipango yake.**



**2022, Tanzania itafanya zoezi la Sensa ambalo mara ya mwisho lilifanyika nchini mwaka 2012, ambapo Tanzania ilikadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni**

# 40



# ANNE MAKINDA AIPA THAMANI SENSA



**KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022, Anne Makinda amelipa thamani zoezi la Sensa kwa mwaka huu, ambalo limepangwa kufanyika Agosti**

# 23

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022, Anne Makinda amelipa thamani zoezi la Sensa kwa mwaka huu, ambalo limepangwa kufanyika Agosti 23, nchi nzima.

Makinda ambaye ni Spika wa zamani aliwaambia watanzania kuwa zoezi la sensa ni la thamani na linapaswa kupewa thamani hiyo na wananchi wote.

Aliweka wazi kuwa thamani hiyo inapaswa kulindwa kwa kiwango kikubwa na wananchi na njia pekee ya kulifanikisha hilo ni kila mmoja kuwa tayari kuhesabiwa.

Kamishna huyo alisema kuwa maandalizi yote kwa ajili ya shughuli hiyo yamekamilika ikiwa ni pamoja nyenzo za mifumo ya Teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA).

Nyenzo hizo zilishafanyiwa majaribio kati ya Septemba 11 hadi 13, 2021 katika mikoa 18 iliyotengwa kwa ajili ya sensa ya watu na makazi ya majaribio , ikiwemo mitano ya Zanzibar na kwa Tanzania Bara ni Mikoa 13. Alisema ipo haja kwa wananchi kutoa ushirikiano mkubwa kwa mawakala wa sensa, Makinda aliwaomba wananchi kutoa taarifa sahihi kwa kila swali litakalo ulizwa pasipo kuwa na udanganyifu wowote ili Serikali ipate taarifa sahihi kuhusu watu na makazi, lakini pia sensa ni siri na mawakala hao wameapa kutunza siri.

"Zoezi la sensa ni la siri na litafanyika kwa siri, tunaomba muondoe hofu" alisema Makinda.

Akizungumzia lengo la zoezi la sensa ya watu na makazi, Kamisaa Makinda alisema ni kutambua idadi ya watu nchini, kujua ubora wa nyumba, kiwango cha umaskini na maendeleo, lakini pia nyumba kupewa anuani kwa lengo la kutambua wakazi wa kaya husika.

## OMBI KWA VIONGOZI WA DINI

Makinda pia amewaomba viongozi wa dini kupitia Jumuiya ya Maridhiano kuwahamasisha watanzania kushiriki kikamilifu zoezi la sensa ya watu na makazi.

Amesema anaamini viongozi wa Jumuiya hiyo watasaidia serikali katika kuhamasisha watanzania kujitokeza kwa wingi kwenye zoezi la uandikishaji wa sensa.

Viongozi wa dini wananafasi kubwa ya kushawishi na kuwahamasisha watu kujitokeza kwa wingi ili kushiriki zoezi hilo muhimu kwa maenedelo ya taifa.

Aliwataka watanzania kutoa ushirikiano katika utoaji wa majibu sahihi kwa watumishi watakaowandikisha huko majumbani na maeneo mengine ili kupata idadi kamili ya watu na makazi yao.

## MIZENGO PINDA ATOA NENO JUU YA SENSA

Kwa upande wake waziri mkuu mstaafu Mizengo Pinda amezitaka familia ambazo zina Watoto wenye ulemavu kutofichwa pindi zoezi la uandikishaji wa sensa utakapofika.

Tabia ya kuwaficha watu hao itasababisha serikali kutowatambua watu wake.

"Serikali itashindwa kufikia malengo yake ya bajeti itakayopangwa kwa ajili ya maendeleo ya watanzania na pia inawanyima haki yao ya kimsingi ya kuhesabiwa kama ilivyo kwa watu wengine.

Itasikitisha kama kutatokea familia zenye watu ambao wanaishi na ulemavu halafu wakawaficha na kusababisha wasihesabiwe, jamani hao nao ni watu kama sisi tulio wazima hivyo nitoe rai kwa familia hizo ziwe tayari kutoa idadi kamili ya watu wanaoishi nao.

> "Zoezi la sensa ni la siri na litafanyika kwa siri, tunaomba muondoe hofu

# NUKUU
# za Anne Makinda







**01**

**Ikiwa mtu ana mke zaidi ya mmoja siku ya kuhesabiwa, atahesabiwa sehemu moja tu aliyolala.**

**02**

**Kila atakae amka ndani ya nchi yetu hata kama sio mtanzania atahesabiwa hata kama ni mgeni tu amekuja kukutembelea kutoka taifa jengine nae atahesabiwa.**

**03**

**Wababa wawape nafasi wakina mama kusema vitu vyao, anaweza akatoa taarifa kwamba mimi nimezaa Watoto lakini wengine wamezaliwa na mtu mwengine.**



# Ripoti ya Sensa ya watu na makazi 2012

**SENSA ya watu na makazi ya mwaka 2022 msingi wake ni sensa ya mwaka 2012 ambayo ilikamilika kwa watu**

# 44,928,923



SENSA ya watu na makazi ya mwaka 2022 msingi wake ni sensa ya mwaka 2012 ambayo ilikamilika kwa watu 44,928,923 kuhesabiwa Bara na Zanzibar, huku idadi ya wanaume ikiwa ni 21,869,990 na wanawake 23,058,933.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Serikali Machi, 2013, ilionesha kuwa katika idadi hiyo ya mwaka 2012 jumla ya Wazanzibari walikuwa 1,303,569, wanaume wakiwa 630,677 na wanawake walikuwa 672,892, huku kwa upande wa Bara watu 43,625,354 wakihesabiwa, wanawake wakiwa 22,386,041 na wanaume ni 21,239,313.

Takwimu zilionesha kuwa ukuaji wa ongezeko la watu kwa mwaka 2002-2012 kwa Tanzania ni wastani wa 2.7 kwa mwaka, huku kwa upande wa Bara ukuaji wake kwa mwaka ukiwa ni wastani wa 2.7 na kwa Zanzibar ikiwa ni 2.8.

Idadi ya makazi kwa Tanzania nzima yalikuwa ni 9,362,758 huku Bara ikiwa na nyumba 9,109,150 na Zanzibar nyumba 253,608. Wastani wa ukubwa wa nyumba kwa Tanzania ulikuwa ni 4.8, kwa Bara ulikuwa ni 4.8 na Zanzibar ni 5.1.

Kiwango cha msongamano wa watu kwa Tanzania kilikuwa 51,

**Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ilidhihirisha kuwapo kwa kasi ya ongezeko la watu**

Bara kikiwa 49 na Zanzibar kikifikia 530, uwiano wa jinsia kwa Tanzania ulikuwa 95, Bara ikiwa na uwiano wa 95 na Zanzibar 94.

Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ilidhihirisha kuwapo kwa kasi ya ongezeko la watu kutoka 12,313,469 waliohesabiwa mwaka 1967 hadi kufikia watu 44,928,923 waliohesabiwa mwaka 2012.

Hii ilidhihirisha kuwa kumekuwa na ongezeko la watu mara tatu zaidi ya ilivyokuwa mwaka 1967. Takwimu zinaonesha mwaka 1978 idadi ya watu ilikuwa milioni 17.5, mwaka 1988 walihesabiwa watu milioni 23.1 na mwaka 2002 walihesabiwa watu milioni 34.4.

## SENSA KIMKOA 2012

Wakati wa zoezi la sensa la mwaka 2012 Tanzania ilikuwa na mikoa 30, kati ya hiyo Zanzibar ilibeba mikoa mitano na Bara ilibeba mikoa 25, mkoa wa Dar es Salaa ulitajwa kubeba asilimia 10 ya idadi ya watu wote wa Bara waliohesabiwa katika kipindi hicho.

Watu waliohesabiwa katika mkoa huo walikuwa ni milioni 4.36, ukifuatiwa na Mwanza watu milioni 2.77, Mbeya milioni 2.71, Kagera watu milioni 2.46, Tabora watu milioni 2.29, Morogoro watu milioni 2.22, Kigoma watu milioni 2.13, Dodoma watu milioni 2.08 na Tanga walihesabiwa watu milioni 2.05.





NMB
Karibu yako
Lango la
Usafirishaji
Kuvuka
Mipaka
P64
MSHIRIKA wa Serikali katika
kujenga TAIFA bora zaidi!
Fanya malipo
ya Serikali
NMB Wakala
Tawi la NMB
NMB Mkononi
Piga *150*66# au Pakua APP
Download on the
App Store
GET IT ON
Google Play
www.nmbbank.co.tz

**Ripoti ya Sensa na makazi ya mwaka 2012 ilionesha kuwapo kwa tofauti ya asilimia moja kati ya wanawake na wanaume, ambapo kwenye asilimia 100, wanawake walionekana kuwa wengi kwa asilimia 51 huku wanaume wakiwa asilimia 49.**

Aidha kulikuwa na mikoa minne ilikuwa na idadi ya watu ya chini ya milioni moja ambayo ni Katavi watu 564,604, Njombe watu 702,097, Lindi watu 864,652 na Iringa watu 941,238.

Kwa upande wa Zanzibar mkoa uliokuwa na idadi kubwa ya watu ni Mjini Magharibi, ambao ulibeba watu 593,678 ambayo ni sawa na asilimia 46 ya idadi ya watu wote wa Zanzibar. Mkoa uliokuwa na idadi ndogo ya watu ulikuwa ni Kusini Unguja ambao ulikuwa na watu 115,588, katika kipindi cha miaka 10 kutoka 2002 hadi 2012 ongezeko la watanzania lilikuwa kwa asilimia 30 kutoka watu milioni 34.4 hadi 44.9 milioni. Ripoti ya Sensa ya mwaka 2012 inaweka wazi kuwa kwa kasi ya sasa ya ukuaji wa ongezeko la watu la asilimia 2.7, idadi ya watu itakuwa mara mbili zaidi ya ilivyo sasa katika miaka 26 ijayo.

## MSONGAMANO WA WATU

Ripoti ya sensa ya mwaka 2012 inaonesha kuwa Tanzania kwa ujumla, watu 51 wamesongamana kwenye eneo la Kilomita moja ya mraba, huku Dar es Salaam ikiwa na watu 3,133 waliosongama kwenye eneo la Kilomita moja ya mraba na Mjini Magharibi ikiwa na watu 2,581 kwa Kilomita moja ya mraba.

Mikoa yenye idadi ndogo ya watu waliosongamana ni Katavi ambayo inakusanya watu 12 kwenye kila kilomita moja ya mraba na Lindi ambayo inabeba watu 13 kwenye kila Kilomita moja ya mraba.

## UKUBWA WA MAKAZI

Ukubwa wa makazi kwa Tanzania ni kama umesalia kuwa ule ule uliopatikana kwenye sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 ambao ulikuwa ni 4.9 kwa nyumba na 4.8 mwaka 2012.

Hata hivyo mikoa 14 ilionekana kuwa na kiwango cha juu cha kitaifa cha ukubwa wa makazi ambao ni 4.8 kwa nyumba, huku mkoa wa Mtwara ukirekodiwa kuwa na kiwango cha chini cha ukubwa wa nyumba ambacho kilikuwa ni 3.7.

## UWIANO WA KIJINSIA

Ripoti ya Sensa na makazi yam waka 2012 ilionesha kuwapo kwa tofauti ya asilimia moja kati ya wanawake na wanaume, ambapo kwenye asilimia 100, wanawake walionekana kuwa wengi kwa asilimia 51 huku wanaume wakiwa asilimia 49.

Hali hiyo ilionesha kuwa uwiano wa wanawake na wanaume kwa Bara ni wanawake 100 kwa wanaume 95, huku mchanganuo huo ukionesha kuwa wastani wa uwiano kwa wanawake na wanaume kwa upande wa Zanzibar ni wanawake 94 kwa wanaume 100.

Kwa mkoa wa Njombe takwimu zilionesha wanaume 88 kwa wanawake 100, Manyara na mikoa mingine mingi ilionekana ni wastani wa wanawake 100 kwa wanaume 92 hadi 95.

Uwiano wa jinsia wa mwaka 1988 hadi 2012 unaonesha uwapo wa idadi kubwa ya wanawake kwa Tanzania Bara na Zanzibar.


1978
idadi ya watu
ilikuwa milioni
17.5
1988
walihesabiwa
watu milioni
23.1
2002
walihesabiwa
watu milioni
34.4
2012
idadi ya watu
ilikuwa milioni
44,928,923
HII ILIDHIHIRISHA
KUWA KUMEKUWA NA
ONGEZEKO LA WATU
MARA TATU ZAIDI YA
ILIVYOKUWA MWAKA
1967

Sensa 2022 KWA MAENDELEO ENDELEVU

# MAENEO MUHIMU 21 YALIYOBAINIKA KWENYE SENSA YA 2012

**Agosti 23, 2022, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya zoezi la sita la Sensa ya Watu na Makazi, sensa ya mwaka huu ilitanguliwa na sensa kama hiyo iliyofanyika Agosti 26, 2012.**

**Takwimu za sensa ya mwaka 2012 zimeonesha kuwa wastani wa asilimia 1.2 ya wamiliki wa nyumba nchini wanaishi nje ya nchi**

# DIASPORA





**Jumla ya watanzania wanaoishi nje ya nchi Diaspora ni**

# 421,456

Agosti 23, 2022, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya zoezi la sita la Sensa ya Watu na Makazi, sensa ya mwaka huu ilitanguliwa na sensa kama hiyo iliyofanyika Agosti 26, 2012.

Sensa ya mwaka 2012 ilikuwa Sensa ya tano baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964.

Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988 na 2002, madhumuni ya kimsingi ya sensa ya 2012 na hata ya mwaka 2022 ni kutoa taarifa juu ya ukubwa , usambazaji, muundo na sifa zingine za kijamii na kiuchumi za idadi ya watu, pamoja na taarifa juu ya hali ya makazi.

Sensa ya mwaka 2012 ilihusisha pia kukusanya taarifa kuhusu upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kama vile shule na hospitali.

Taarifa iliyotolewa ni muhimu kwa ufuatiliaji na kutathmini mipango ya maendeleo ya nchi.

Ripoti ya serikali iliyotolewa mwaka 2014 ya sensa ya mwaka 2012, ilionesha wasifu wa msingi wa idadi ya watu, masuala ya kijamii na kiuchumi.

Ripoti hiyo ambayo imesheheni majedwali inatoa uchanganuzi mfupi wa maelezo yanayohusu maeneo makuu yaliyoangaziwa katika sensa hiyo.

Maeneo 21 ambayo yaliangaziwa katika ripoti hiyo ni pamoja na ukubwa na ukuaji wa idadi ya watu, mgawanyo wa umri na jinsia; muundo wa kaya, hali ya ndoa, ulemavu, uraia, usajili wa kuzaliwa na Diaspora.

Mada nyingine ni uzazi na vifo, uhai wa wazazi, kusoma na kuandika na elimu, shughuli za kiuchumi, hali ya makazi, umiliki wa mali, huduma za kaya, kilimo na mifugo; na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Ripoti hiyo imetoa muhtasari wa misingi wa idadi ya watu, masuala ya kijamii na kiuchumi. Maeneo muhimu yaliyoangaliwa ni:-

## KUONGEZEKA KWA MAKAZI MIJINI

Idadi ya makazi kwa mijini imeongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2002 hadi asilimia 33 mwaka 2012 huku hali ikiwa tofauti vijijini, ambapo yamepungua kutoka asilimia 74 mwaka 2002 hadi asilimia 67 mwaka 2012.

**Idadi ya makazi kwa mijini imeongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2002 hadi asilimia 33**



Kwa upande wa Zanzibar, makazi yameongezeka kutoka asilimia 39 hadi asilimia 45 mijini katika kipindi cha miaka 10 kutoka 2002 hadi 2012, hali ikiwa tofauti kwa vijijini ambapo imepungua kutoka asilimia 61 mwaka 2002 hadi asilimia 55 mwaka 2012.

Kuongezeka kwa kaya katika maeneo ya mijini kunaweza kuhusishwa na uhamiaji mijini na uainishaji upya wa baadhi ya maeneo ya vijijini hadi mijini katika miaka ya hivi karibuni.

## WANAWAKE VIONGOZI WA MAKAZI

Sensa ya mwaka 2012 ilionesha kuwa moja ya tatu ya wanawake ndio wanasimamia na kuongoza familia zao, kiwango hicho ni sawa na asilimia 33.4 ya makazi yote nchini.

Hali hiyo itaendelea kwa muongo mmoja zaidi,

Ilibainika zaidi kuwa wastani wa kaya zinazoongozwa na wanawake ni mara mbili (watu 7.3) kuliko wa kaya zinazoongozwa na wanaume (watu 3.5).

Aidha umasikini umetajwa kuwa sababu ya watu kuzaliana sana.

## NDOA ZA UTOTONI

Asilimia 58 ya watu waliohesabiwa mwaka 2012 ambao wana umri wa miaka 15 na zaidi wako kwenye ndoa ama wanaishi kinyumba.

Kiwango kikubwa cha wanaoishi kwenye ndoa ni watoto wa kike ambao ni asilimia 58 tofauti na ilivyo kwa wanaume ambao ni asilimia 57.

Hata hivyo kiwango hicho kimetajwa kupungua kutoka asilimia 54 mwaka 2002 hadi asilimia 51 mwaka 2012.

Ripoti imeweka wazi kuwa hali hiyo inaweza kuchangia athari za VVU/UKIMWI na matatizo ya kiuchumi.

Matokeo pia yanaonyesha asilimia ya watu waliotengana au waliotalikiana ilipungua kutoka asilimia tano (5) mwaka 2002 hadi asilimia nne mwaka 2012 ikionyesha utulivu wa ndoa kwa muda.

Matukio ya wajane katika ngazi ya kitaifa yamepungua kutoka asilimia 5 mwaka 2002 hadi asilimia 3 mwaka 2012.

## UMRI WA NDOA

Ripoti inaonesha uwapo wa mabadiliko kwenye umri wa ndoa, awali umri wa wastani wa kuolewa kwa kwa wanawake ulikuwa miaka 21 mwaka 2002, katika sensa ya mwaka 2012 ilionesha umri umeongezeka kidogo na kuwa miaka 22.

Wastani wa umri wa kuoa kwa wanaume ulisalia kuwa wa miaka 26 kama ilivyokuwa kwenye sensa ya mwaka 2002 na sensa ya 2012.

Sensa ya mwaka 2012 imeonesha kuwa wastani wa umri wa ndoa ulikuwa juu kidogo kwa Zanzibar kuliko Bara kwa wanaume na wanawake.

Kwa ujumla, ongezeko hilo la umri wa ndoa linatajwa kuchangiwa na kuongezeka kwa kiwango cha elimu kwa wanaume na wanawake

**Wastani wa umri wa kuoa kwa wanaume ulisalia kuwa wa miaka 26 kama ilivyokuwa kwenye sensa ya mwaka 2002 na sensa ya 2012.**

## VYETI VYA KUZALIWA

Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 ni asilimia 13 tu ya watanzania wote ndio wanamiliki vyeti vya kuzaliwa. Kwenye takwimu hizo wanaume wanaonekana kuongoza kwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa kwa asilimia 16 huku wanawake wakiwa ni asilimia 15.

Kwa Zanzibar hali imeonekana kuwa tofauti, ambapo asilimia 71 ya watu wanaonekana kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Hatua hiyo imechangiwa na utaratibu wa muda mrefu wa Zanzibar wa kusajili watoto wanapozaliwa tofauti na Bara, ambayo imeanza utaratibu huo mwaka 2002.

## DIASPORA

Takwimu za sensa ya mwaka 2012 zimeonesha kuwa wastani wa asilimia 1.2 ya wamiliki wa nyumba nchini wanaishi nje ya nchi, jumla ya watanzania wanaoishi nje ya nchi Diaspora ni 421,456.



**Makazi yanayomilikiwa na Diaspora Tanzania ni 111,670, vijijini ni 54,652, mijini ni 57,018, Bara ni makazi 107,021, vijijini ni 53,740 na mijini ni 53,281. Kwa Zanzibar ni makazi 4,649, vijijini zikiwa nyumba 912 na mijini ni nyumba 3,737.**

Kwa Zanzibar asilimia mbili ya nyumba zinamilikiwa na watu wanaoishi nje ya nchi. Makazi yanayomilikiwa na Diaspora Tanzania ni 111,670, vijijini ni 54,652, mijini ni 57,018, Bara ni makazi 107,021, vijijini ni 53,740 na mijini ni 53,281. Kwa Zanzibar ni makazi 4,649, vijijini zikiwa nyumba 912 na mijini ni nyumba 3,737.

## KUJUA KUSOMA NA KUANDIKA

Elimu ya watu wazima (watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi) nchini Tanzania ni asilimia 78, wanaume waliokuwa wanajua kusoma na kuandika ni asilimia 83 tofauti na wanawake ambao ni asilimia 73.

Hali ni hivyo hivyo kwa Tanzania bara na Tanzania Zanzibar. Kiwango cha elimu ya watu wazima nchini Tanzania kiliongezeka kutoka asilimia 69 mwaka 2002 hadi asilimia 78 katika sensa ya mwaka 2012.

## ELIMU YA MSINGI

Uwiano wa uandikishaji wanafunzi kwa shule za msingi umeongezeka kidogo kwa asilimia 77, kwa upande wa wanawake umefikia asilimia 78 huku wanaume wakiandikishwa kwa asilimia 75.

Ripoti imeonesha uandikishaji wa jumla umepanda zaidi kwa Zanzibar, ambao umefikia asilimia 86 tofauti na Bara ambako ni asilimia 77.

Kiwango cha uandikishaji kwa Bara na Zanzibar kimeongezeka kutoka asilimia 69 mwaka 2002 hadi asilimia 77 mwaka 2012.

## SHUGHULI ZA KUONGEZA KIPATO

Shughuli kuu ya kuwaingizia kipato watanzania wengi ni kilimo, takwimu zinaonesha wakulima ni asilimia 62 wakifuatiwa na wafanyakazi ambao ni asilimia 6.

## ULEMAVU

Takwimu za Sensa ya mwaka 2012 zinaonesha ulemavu unaowasumbua wengi ni uoni hafifu, tatizo hili limetajwa kuwasumbua watu wengi, ambapo asilimia 1.9 walilitaja tatizo hilo likifuatiwa na tatizo la miguu ambalo ni asilimia 1.2, usikivu hafifu ni asilimia 1.0 na chini ya asilimia 0.04 ya watanzania ni walemavu wa ngozi. Hakuna tofauti kubwa ya idadi ya walemavu kwa Bara na Zanzibar.

## UBORA WA MAJENGO

Kumekuwa na mabadiliko makubwa katika ujenzi wa nyumba mijini na vijijini, ambapo sensa ya mwaka 2012 imebaini kuwa idadi kubwa ya watu wanajenga majengo ya kisasa.

Asilimia 65 ya watu wanaojenga wanatumia mabati, tofauti na ilivyokuwa mwaka 2002 ambapo waliokuwa wakitumia mabati ni asilimia 46. Aidha matumizi ya saruji, vigae, tarazo na mbao zilizong'arishwa kwenye sakafu yameongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2002 hadi asilimia 39 mwaka 2012.

Hatua hii ya maboresho katika ujenzi yanadhihirisha wazi ukuaji wa uchumi kwa nchi na kwa mtu mmoja mmoja.

## MATUMIZI YA UMEME

Matumizi ya umeme kama njia kuu ya nishati ya mwanga

**Kumekuwa na mabadiliko makubwa katika ujenzi wa nyumba mijini na vijijini, ambapo sensa ya mwaka 2012 imebaini kuwa idadi kubwa ya watu wanajenga majengo ya kisasa.**

yameongezeka , wastani wa asilimia 49 ya makazi yaliyopo mijini yameunganishwa na umeme ukilinganisha na ilivyokuwa mwaka 2002 ambapo yalikuwa ni aslimia nane tu. Matumizi ya umeme kwa Zanzibar ni makubwa kwa asilimia 43, huku Bara ikiwa ni asilimia 21.

## MATUMIZI YA MAJI

Asilimia 37 ya makazi binafsi Tanzania nzima yameunganishwa na mabomba ya maji safi na salama, kwa mijini ni asilimia 59 ikiwa ni mara mbili ya vijijini ambako ni wastani wa asilimia 26.

Kwa Zanzibar asilimia 73 ya nyumba zimeunganishwa na maji safi ya kunywa huku Bara ikiwa ni asilimia 36.

## HUDUMA YA CHOO

Sensa ya mwaka 2012 imeonesha kuwa asilimia 76 ya nyumba binafsi Tanzania zinatumia vyoo vya mashimo.



Kwa upande wa Bara nyumba zenye vyoo hivyo ni asilimia 77 na asilimia 43 kwa Zanzibar. Aidha asilimia nane ya nyumba hazina vyoo na kwa Zanzibar ni asilimia 19.

## TAKA TAKA

Takwimu za sensa za mwaka 2012 zimeonesha kuwa robo tatu ya makazi ya mijini hayana njia sahihi za kuhifadhi takataka. Ni asilimia 36 tu ndio wamechimba mashimo huku asilimia 63 wakizitupa kwenye vichaka au kwenye maeneo ya wazi.

## UMILIKI WA MALI

Sensa ya mwaka 2012 imeonesha kuwa asilimia 70 ya Watanzania wanamiliki ardhi au mashamba, asilimia 75 wanamiliki nyumba, asilimia 64 wanamiliki simu za mikononi na asilimia 62 wanamiliki redio. Umiliki wa simu za mikononi kwa Zanzibar ni asilimia 80 na Bara ni asilimia 63

## MIFUKO YA HIFADHI ZA JAMII

Takwimu za mwaka 2012 zinaonesha kuwa asilimia 13 ya makazi nchini Tanzania, angalau mwanakaya mmoja ni mwanachama wa mifuko ya jamii. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya wa Jamii (CHF) ndio imetajwa sana kwa asilimia sita

**Matokeo ya sensa ya mwaka 2012 yameonesha kuongezeka kwa kiwango cha umri wa kuishi kutoka miaka 50 mwaka 1988 hadi kufikia miaka 61 mwaka 2012.**

## UZAZI WA MPANGO

Sensa ya mwaka 2012 imeonesha kupungua kwa kasi ya uzazi kutoka asilimia 6.5 mwaka 1988 hadi asilimia 5.2 mwaka 2012, hatua hiyo imechangiwa na kuongezeka kwa kiwango cha umri wa mwanamke kuolewa, matumizi ya kisasa ya uzazi wa mpango na kukua kwa kiwango cha elimu kwa wanawake wengi.

## KIWANGO CHA KUISHI

Matokeo ya sensa ya mwaka 2012 yameonesha kuongezeka kwa kiwango cha umri wa kuishi kutoka miaka 50 mwaka 1988 hadi kufikia miaka 61 mwaka 2012. Matokeo hayo yameonesha mwanamke ameongeza umri wa kuishi hadi kufikia miaka 63 huku mwanaume akifikia miaka 60.

## VIFO VYA WATOTO

Matokeo ya awali ya sensa ya mwaka 2012 juu ya vifo vya watoto wachanga yalionesha kuwa katika kila watoto wachanga 1000 watoto 45 hufariki dunia. Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilikuwa cha juu kwa wanaume kuliko watoto wachanga wa kike. Vile vile kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilichozingatiwa kwa wanaume kilikuwa vifo 51 kwa kila watoto 1000 ikilinganishwa na vifo 42 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai kwa wanawake. Matokeo hayo yalidhihirisha zaidi kuwa kiwango cha vifo vya watoto wachanga nchini Tanzania kimepungua kutoka vifo 115 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa wakiwa hai mwaka 1988 hadi vifo 45 kila watoto 1000 mwaka 2012.

## VIFO VYA WAJAWAZITO

Sensa ya mwaka 2012 imeonesha kuwapo kwa mafanikio makubwa ya serikali kupambana na vifo vya wajawazito, inakadiriwa kuwa katika wajawazito 100,000 ni wajawazito 432 ndio hufariki dunia, hii ikimaanisha katika wajawazito 1,000 ni wajawazito wanne ndio hufariki dunia. Takwimu hizo za vifo vya wajawazito zimeanza kuchukuliwa kwenye sensa ya mwaka 2012 hali inayofanya mlinganisho wa suala hilo uanzie mwaka 2004/5 ambapo vifo vya wajawazito vilikuwa 578 kwenye kila wajawazito 100,000.


USIKOSE KUSOMA
TOLEO LIJALO LA
Royal tour

KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## SENSA NI MSINGI WA MAENDELEO

KATIKA kuendeleza zoezi la kuwaletea maendeleo Watanzania, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendesha zoezi la sita la kuhesabu watu wake sanjari na makazi. Kimsingi zoezi hili linajulikana kama Sensa ya Watu na Makazi.

Sensa ya kwanza ya Tanzania ilifanyika mwaka 1967, ikiwa ni miaka sita baada ya Uhuru, ingawa kulikuwa na changamoto kadhaa, lakini zoezi hilo lilikamilika vema na Watanzania 12,313,469 walihesabiwa.

Tangu hapo hadi kufikia mwaka 2012 ilipofanyika sensa ya tano, kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu mara nne zaidi ya ile iliyopatikana mwaka 1967.

Hatua hii inadhihirisha wazi kuwapo kwa kasi ya ongezeko la watu mijini na vijijini, hali inayoibua umuhimu wa zoezi la Sensa la mwaka huu ili kuipa Serikali nafasi ya kujua namna gani itapanga mipango yake ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake.

TZ&BEYOND tunaamini Sensa ni msingi wa maendeleo, nchi isiyojua idadi ya watu wake, kamwe haiwezi kujipanga na kama itajipanga, basi itawanufaisha wachache huku wengi wakiachwa bila kufikishiwa maendeleo.

Ikumbukwe kuwa, zoezi la kuhesabu watu si la Tanzania pekee bali nchi nyingi duniani, zimekuwa zikifanya zoezi hili kwa miaka tofauti tofauti. Nchi zilizoendelea, hutekeleza zoezi hili kila baada ya miaka mitano ingawa nchi nyingine hufanya Sensa kila baada ya miaka 10 kama inavyofanya Tanzania.

Hata hivyo, zipo nchi zinazochelewa zaidi kufanya Sensa kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kivita kama ilivyo kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo-DRC ambayo ilitekeleza zoezi hilo kwa mara ya mwisho mwaka 1984. Inaelezwa nchi hiyo imeshindwa kutekeleza zoezi hilo kwa muda mrefu kutokana na hali tete ya usalama nchini humo.

Kutofanyika kwa sensa, kunaweza kusababisha umasikini ingawa zoezi hili litafanyika kwa muda mfupi, matokeo yatakayopatikana yawe chanya au hasi, yataishi kwa miaka 10 hadi kufikia mwaka 2032.

Katika kipindi chote hicho, matokeo yatakayopatikana kwenye sensa ya 2022, ndiyo msingi wa upangaji wa mipango ya Serikali ya muda mfupi, muda wa kati na hata muda mrefu.

Rai yetu kwa wananchi wa Tanzania, watoe ushirikiano kwa watu waliopewa jukumu la kukamilisha zoezi hilo la kuhesabu watu.

Sensa haina madhara kwa mwananchi mmoja mmoja ama kwa nchi, tunajua ipo dhana kuwa suala la kuhesabiwa lina nia ya kupunguza kasi ya kuzaliana, hili halina ukweli, sensa ina faida kubwa kuliko hasara.

Sensa ni kwa maendeleo ya Taifa, tujiandae kuhesabiwa.





**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**

TRA
TANZANIA REVENUE AUTHORITY
ISO 9001: 2008 Certified

VISION PLUS
EYE CLINIC

KCB BANK

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK
Tunakusikiliza

NMB

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

TIB CORPORATE BANK
Your Partner Bank

TADB
Tanzania Agricultural Development Bank
"The Farmers' Bank"

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# SHUKRANI

za dhati kwa WASHIRIKA WETU




# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

The bank that listens